Kioo cha Lugha, Juz. 24(1), 40-49
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v24i1.3

Uhusiano kati ya Semantiki na Pragmatiki katika Lugha

Tumaini Mahendeka[1]

Ikisiri

Semantiki na pragmatiki ni matawi ya isimu yanayochunguza maana ambayo yana uhusiano wa karibu kutokana na kutegemeana kwake katika kufasiri na kuelewa matumizi ya lugha. Lengo la makala hii ni kufafanua uhusiano uliopo kati ya semantiki na pragmatiki katika lugha. Data katika makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini na zilichambuliwa kwa mkabala wa kitaamuli kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui. Makala hii ilitumia Nadharia ya Maana ni Matumizi iliyoasisiwa na Ludwig Wittgenstein (1953) katika kazi yake ya *Philosophical Investigation*. Matokeo yanaonesha kwamba semantiki na pragmatiki zina uhusiano wa karibu kwa kuwa yote ni matawi ya isimu katika lugha ambayo yanashughulikia maana. Pia, maana za kisemantiki huibua maana za kipragmatiki na matawi yote huhawilisha ujumbe katika mawasiliano. Aidha, matawi yote huchunguza maana za ishara kwa kutumia simiotiki.

1.0 Utangulizi

Lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano katika jamii, na uchunguzi wa maana ndiyo msingi wa taaluma ya isimu. Katika muktadha huo, semantiki na pragmatiki ni matawi muhimu ya isimu yanayojihusisha na uchambuzi wa maana katika lugha, ingawa hutofautiana katika kiwango cha uchambuzi. Semantiki ni tawi la isimu linalochunguza maana ya kiisimu[2] kama ilivyosimbwa ndani ya mfumo wa lugha bila kuzingatia muktadha wa matumizi. Kwa mujibu wa Griffiths (2006), Saeed (2016), Yule (2006) na Fromkin, Rodman, Hyams, Amberber, Cox na Thornton (2022) semantiki huchunguza maana katika viwango mbalimbali vya lugha kama mofimu, maneno, virai na sentensi kwa kuzingatia uhusiano kati ya umbo la lugha na maana yake ya msingi.

Pragmatiki ni tawi la isimu linalochunguza matumizi ya lugha katika muktadha wa mawasiliano. Kwa mujibu wa Kreidler (1998), Bublitiz na Norrick (2011) na Katui (2021), pragmatiki huchunguza maana ya mzungumzaji, yaani kile kinachokusudiwa katika usemi kulingana na mazingira ya kijamii na kimawasiliano. Semantiki na pragmatiki hutofautishwa kielimu katika kiwango cha uchambuzi kwani semantiki hushughulikia maana ya kiisimu iliyo thabiti ndani ya mfumo wa

[1] Mkuza Mitaala, Kitengo cha Uthibiti Ubora, Taasisi ya Elimu Tanzania, Tanzania.
Baruapepe: tumaini.mastajabu@tie.go.tz

[2] Maana ya kiisimu ni maana ya kisemantiki

lugha ilhali pragmatiki hushughulikia maana inayobadilika kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa hiyo, semantiki na pragmatiki ni matawi tofauti ya isimu kwa misingi ya uchambuzi lakini yanategemeana katika utendaji, yaani ujenzi wa maana katika mawasiliano ya lugha.

Kutokana na tafiti mbalimbali, semantiki na pragmatiki ni matawi tofauti ya lugha lakini yana uhusiano wa karibu na yanakamilishana kiutendaji. Mgawanyo wake kama matawi mawili unatokana na tofauti ya kiuchambuzi na kinadharia. Semantiki hushughulikia maana iliyosimbwa katika mfumo wa lugha bila kuzingatia muktadha ilhali pragmatiki huchunguza maana inayotokana na matumizi ya lugha katika muktadha halisi wa mawasiliano. Hivyo, utofauti huu si wa kiutendaji bali ni mkakati wa kiuchambuzi unaolenga kurahisisha uchunguzi wa maana katika viwango tofauti vya lugha. Kwa mantiki hiyo, matawi haya mawili ni tofauti kwa upeo wa uchambuzi lakini ni kamilishani katika utendaji wake. Kwa mujibu wa Saeed (2016), mipaka kati ya semantiki na pragmatiki si thabiti kwa urahisi kwani maana ya lugha huathiriwa na mwingiliano kati ya maana ya kiisimu na muktadha wa matumizi. Hivyo, wataalamu kama Cruse (2006), Geeraerts (2010) na Kroeger (2018) wanaeleza kuwa ni vigumu kuweka mipaka madhubuti kati ya matawi haya kutokana na kutegemeana kwao kiutendaji katika matumizi ya lugha. Ingawa tafiti mbalimbali zimechunguza semantiki na pragmatiki, bado kuna mjadala kuhusu mipaka na uhusiano kati ya matawi haya mawili hususani katika uchambuzi wa lugha za Kiafrika kama Kiswahili. Tafiti nyingi zimeeleza tofauti za msingi za semantiki na pragmatiki lakini bado kuna haja ya kuchunguza namna matawi haya yanavyokamilishana katika muktadha wa mawasiliano. Hivyo, makala hii inachunguza kwa kina mjadala huo kwa kufafanua uhusiano kamilishani kati ya semantiki na pragmatiki katika muktadha wa Kiswahili.

2.0 Mbinu za Ukusanyaji wa Data na Nadharia ya Utafiti

Utafiti katika makala hii ulikuwa wa maktabani na ulitumia mkabala wa kitaamuli. Data zilikusanywa kupitia uchambuzi wa matini mbalimbali zinazohusu semantiki na pragmatiki katika lugha kwa lengo la kupata ufafanuzi wa kina kuhusu mada ya utafiti. Data hizo zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui huku uchambuzi huo ukitumia

Nadharia ya Maana kama Matumizi iliyoasisiwa na Ludwig Wittgenstein mwaka 1953. Nadharia hii ilitumika kama msingi wa uchambuzi wa data kwa sababu inaeleza jinsi maana katika lugha inavyoweza kubadilika kutokana na muktadha wa mawasiliano. Aidha, nadharia hii ilisaidia kufafanua namna lugha inavyofanya kazi katika viwango vyote viwili, yaani kile kinachosemwa moja kwa moja na kile kinachomaanishwa katika muktadha wa matumizi.

Nadharia hii iliasisiwa na Ludwig Wittgenstein katika kazi yake ya pili ya *Philosophical Investigations* iliyochapishwa mwaka 1953. Kumar (2019) anaeleza kwamba Wittgenstein alibadilisha mawazo yake ya awali katika *Tractatus Logico-Philosophicus* (1921) ambapo aliona maana ya lugha kama uwakilishi wa ukweli.

Katika kazi zake za baadaye hasa *Philosophical Investigations*, Wittgenstein alieleza kuwa maana ya neno haipo katika uhusiano wake na kitu fulani tu bali jinsi linavyotumiwa ndani ya michezo ya lugha. Wittgenstein alitambua maana kutokana na matumizi ya neno. Hivyo, aliandika maana ya neno kuwa ni matumizi yake katika lugha, na matumizi ya neno hilo kwa vitendo ndiyo maana yake. Ni dhahiri kwamba katika kuelezea jinsi neno linavyotumiwa, tunaelezea maana yake na kujua maana yake ni sawa na kujua jinsi ya kuitumia. Mwanafalsafa Ludwig Wittgenstein katika miaka ya 1930 alieleza kuwa maana ya neno ni matumizi yake katika lugha. Watoto hujifunza maana ya viambolugha kutokana na jinsi viambo hivyo vitumiwavyo na wanalugha na jinsi wao wenyewe watumiavyo viambo hivyo katika kuwasiliana na wana lugha hao. Kahigi (2019) anaeleza kuwa Nadharia ya Maana kama Matumizi inadai kuwa maana ya neno ni matumizi yake katika lugha kwani inawezekana kabisa kuzungumza matumizi ya neno lolote lile.

Msingi mkuu wa nadharia hii ni maana ni matumizi kwani maana ya neno hutokana na matumizi yake. Hivyo, pragmatiki hutumia maana za kisemantiki kurejelea maana za kimkutadha, jambo linalofanya matawi haya mawili ya isimu kuwa na uhusiano wa karibu, na kushindwa kutenganishwa kiutendaji. Nadharia hii ilitumika katika utafiti huu kwa sababu inatoa msingi wa kuelewa jinsi maana inavyoweza kubadilika kutoka ile iliyoelezwa na sheria za lugha (semantiki) hadi ile inayoathiriwa na mazingira ya mawasiliano (pragmatiki), na jinsi lugha inavyofanya kazi katika viwango vyote viwili, yaani kile kinachosemwa (semantiki) na kile kinachomaanishwa katika muktadha (pragmatiki).

3.0 Uwasilishaji wa Data

Uchambuzi wa data za utafiti huu unaonesha kuwa semantiki na pragmatiki ni matawi ya isimu yenye uhusiano wa karibu na yanayokamilishana katika kufafanua maana katika lugha. Matokeo yanaonesha kuwa maana ya kisemantiki husaidia kuelewa maana ya msingi ya tungo, huku pragmatiki ikisaidia kufasili maana hiyo kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya lugha. Hali hii ilijitokeza katika mifano mbalimbali iliyochunguzwa ambapo maana ya ujumbe ilieleweka kwa kuzingatia vipengele vya kisemantiki na kipragmatiki.

3.1 Semantiki na Pragmatiki Hujishughulisha na Maana katika Lugha

Semantiki na pragmatiki zote hujihusisha na maana katika lugha. Hata hivyo, kila taaluma hushughulikia maana kwa mtazamo tofauti. Kwa mujibu wa Horn na Ward (2006) pamoja na Birner (2013), semantiki huchunguza maana ya maneno na sentensi kama ilivyosimbwa katika mfumo wa lugha ilhali pragmatiki hujikita katika maana inayotokana na matumizi ya lugha katika muktadha maalumu wa mawasiliano. Kwa hiyo, semantiki hueleza maana za msingi za maneno na sentensi kwa kuzingatia mfumo wa lugha wenyewe wakati pragmatiki huchunguza namna maana hizo zinavyofasiliwa kulingana na mazingira ya matumizi yake. Hivyo,

uhusiano huu kati ya matawi haya mawili ya kiisimu ni wa kiutendaji. Uhusiano huo unajidhihirisha katika Data Na. 1 (a) na (b).

1. *(a) Umesimama mbele ya televisheni.*
   (b) Nje kuna baridi.

Chanzo: Yule (1996: 55)

Kisemantiki, Data Na. 1(a) inamaanisha kuwa mtu fulani amesimama mbele ya televisheni. Maana hii hutokana moja kwa moja na maneno yaliyotumika katika sentensi bila kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Hata hivyo, kipragmatiki, maana ya sentensi hiyo hutegemea muktadha wa mawasiliano. Kwa mfano, ikiwa msemaji alikuwa akitazama televisheni na mtu mwingine akasimama mbele yake, sentensi hiyo inaweza kufasiliwa kama ombi la kumtaka mtu huyo aondoke au asogee pembeni ili asimzuie kutazama televisheni. Pia, kisemantiki, katika Data Na. 1(b) inamaanisha kuwa mtu amehisi baridi ambayo inatokea nje ya nyumba. Hata hivyo, maana ya kipragmatiki katika sentensi ya Data Na. 1(b) hutegemea muktadha wa mawasiliano. Ikiwa msemaji alikuwa anahisi baridi akiwa ndani ya nyumba na madirisha yako wazi ni ombi la kumtaka msikilizaji kufunga madirisha ili baridi isiendelee kwa ndani. Hivyo basi, pragmatiki huonesha maana fiche au dhamira ya msemaji ambayo haijaelezwa moja kwa moja katika tungo yenyewe.

Kutokana na data hiyo, ni wazi kuwa semantiki na pragmatiki hukamilishana katika kufafanua maana katika mawasiliano. Uelewa wa maana hauwezi kukamilika kwa kutegemea maana ya kisemantiki pekee bila kuzingatia muktadha wa matumizi ya lugha. Kwa mujibu wa Yule (1996:3), pragmatiki ni taaluma inayochunguza kile kinachomaanishwa katika mawasiliano zaidi ya kile kinachosemwa moja kwa moja. Kwa msingi huo, pragmatiki huhusika na matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano tofauti na semantiki ambayo hujikita katika maana ya kiisimu isiyotegemea muktadha mahususi.

Vilevile, Hassan (2011) anaeleza kuwa pragmatiki na semantiki ni taaluma zinazopakana kwa sababu zote hujihusisha na maana katika lugha. Hata hivyo, dhana ya “maana” yenyewe huwa na tafsiri tofauti kutegemeana na muktadha wa kiisimu. Anaendelea kufafanua kuwa semantiki huhusisha maana ya kimantiki iliyosimbwa katika mfumo wa lugha ilhali pragmatiki huhusisha maana ya mzungumzaji inayojengwa kupitia muktadha wa usemi.

Aidha, Griffiths (2006) anaeleza kuwa semantiki ni taaluma inayochunguza maana iliyosimbwa katika maneno, virai na sentensi za lugha wakati pragmatiki hujihusisha na namna maana hiyo inavyotumiwa na kufasiliwa katika mazingira halisi ya mawasiliano. Kwa hiyo, pragmatiki huzingatia uhusiano uliopo kati ya lugha, mzungumzaji, msikilizaji na mazingira ya matumizi ya lugha. Tofauti kuu kati ya taaluma hizi ni kwamba semantiki huangalia maana ya kiisimu iliyo ndani ya tungo yenyewe ilhali pragmatiki huangalia maana inayopatikana kwa kuzingatia matumizi ya tungo katika muktadha maalumu wa mawasiliano. Hata hivyo, tofauti hii si ya kiutendaji bali ni ya kiuchambuzi kwa sababu semantiki na pragmatiki

huwakilisha viwango viwili vinavyokamilishana katika uchunguzi wa maana. Maana ya kimuktadha inayochunguzwa na pragmatiki hujengwa juu ya msingi wa maana ya kisemantiki. Hali hii inaonesha kuwa taaluma hizi haziwezi kutenganishwa kabisa kiutendaji bali hutegemeana katika kujenga na kufafanua maana katika lugha.

Kutokana na data na maelezo ya Yule (1996), Harn na Ward (2006), Griffiths (2006), Hassan (2011) na Birner (2013), ni dhahiri kuwa semantiki na pragmatiki zina uhusiano wa karibu kutokana na mtagusano wake kiutendaji katika uchunguzi wa maana katika lugha. Semantiki hutoa msingi wa maana ya lugha ilhali pragmatiki hupanua maana hiyo kwa kuzingatia muktadha, dhamira ya msemaji, maarifa ya pamoja pamoja na hali halisi ya mawasiliano. Kwa hiyo, semantiki na pragmatiki hushirikiana kuhakikisha kuwa maana katika lugha haibaki katika kiwango cha maana ya moja kwa moja pekee, bali pia huzingatia mazingira ya matumizi yake katika jamii.

3.2 Semantiki na Pragmatiki Hutumika Kuhawilisha Ujumbe katika Mawasiliano

Lugha yoyote ile ina maana kwa watumiaji wake wakati wa mawasiliano. Huitumia lugha kuhawilisha ujumbe wakati wa mawasiliano baina yao. Ujumbe unaobebwa katika mawasiliano huwa na maana ama ya kisemantiki au ya kipragmatiki. Semantiki hutoa maana ya msingi ya maneno lakini pragmatiki hutumia muktadha na uelewa wa kijamii kuhakikisha ujumbe unahawilishwa kwa njia sahihi. Hivyo, katika mawasiliano, wazungumzaji wanahitaji kuelewa maana zote mbili kama inavyojidhihirisha katika Data Na. 2.

2. *Kuna baridi hapa.*

Chanzo: Fromkin, Rodman, Hyams, Amberber, Cox na Thornton (2022: 210)

Kulingana na Data Na. 2, kisemantiki, sentensi hii inaeleza ukweli wa moja kwa moja kwamba anahisi baridi katika eneo hilo au hali ya joto katika eneo hilo ni ya chini. Hakuna maana nyingine iliyoongezwa au kuhusishwa na muktadha. Hata hivyo, kutegemeana na muktadha, mzungumzaji wa sentensi hii anaweza kuwa anamwomba mwenzake wahame mahali hapo ili waende katika eneo jingine lenye joto bila kusema moja kwa moja. Pia, kulingana na muktadha, mzungumzaji anaweza kuwa anaomwomba msikilizaji afunge madirisha, azime au awashe kiongezajoto.

Ingawa semantiki na pragmatiki zinatofautiana katika upeo wa uchambuzi, bado zinakamilishana kwa namna inayowezesha tafsiri sahihi ya ujumbe katika mawasiliano kwa kuwa uelewa wa maana ya msingi na maana ya muktadha huchangia kwa pamoja katika kupunguza utata na kuongeza ufanisi wa mawasiliano. Hivyo, semantiki na pragmatiki ni vipengele muhimu vya lugha vinavyoshirikiana kuhakikisha kwamba ujumbe unahawilishwa kwa usahihi katika mawasiliano kwa kuwa semantiki hutoa maana ya msingi ya maneno na miundo ya

sentensi wakati pragmatiki huongeza muktadha na matumizi ya kijamii kutoa maana kamili na sahihi kulingana na hali husika. Hansen (2008) anaeleza kuwa maana ya kipragmatiki ni ile ya tafsiri ukiongeza na ile iliyobaki ambapo maana ya kipragmatiki huchukuliwa kuwa ya kusudio la kimawasiliano la mzungumzaji katika mazingira fulani. Hivyo, matawi haya ya isimu yana uhusiano wa karibu na ni ngumu kuweka mipaka kati yao. Yule (2006) naye anaunga mkono uhusiano huu kwa kueleza kuwa semantiki hutoa maana ya msingi ya maneno lakini pragmatiki hutumia muktadha na uelewa wa kijamii ili kuhakikisha ujumbe unahawilishwa kwa njia sahihi. Kwa mujibu wa Yule (2006), ni dhahiri kuwa semantiki na pragmatiki hutumika kwa pamoja katika kuhawilisha ujumbe katika mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji au mwandishi na msomaji. Uhawilishaji wa ujumbe katika mawasiliano hauhusiani tu na kutambua maana ya maneno bali pia kuelewa kile kinachokusudiwa na mzungumzaji katika mazingira husika. Ili kufanikisha mawasiliano yenye ufanisi, washiriki wanapaswa kuunganisha maarifa ya semantiki (maana ya msingi) na pragmatiki (maana ya muktadha). Kwa mantiki hiyo, bila semantiki, mawasiliano yangekosa maana ya msingi, na bila pragmatiki maana hiyo ingekosa uelekeo unaofaa kulingana na muktadha wa mazungumzo. Mchanganyiko wa semantiki na pragmatiki huwezesha lugha kuwa nyenzo bora ya kueleza mawazo na hisia mbalimbali kwa ufasaha kati ya wazungumzaji na wasikilizaji.

3.3 Maana za Kisemantiki Huchanuza Maana za Kipragmatiki

Maana katika lugha hujengwa kupitia uhusiano wa karibu kati ya semantiki na pragmatiki ambapo semantiki hutoa msingi wa maana ya kiisimu iliyo ndani ya mfumo wa lugha ilhali pragmatiki huipanua au kuibadilisha maana hiyo kulingana na muktadha wa matumizi. Kutokana na uhusiano huo, wanaisimu wengine hubainisha pragmatiki kama mtoto wa semantiki. Maana za kipragmatiki haziwezi kujitegemea bila kuwapo kwa maana ya kisemantiki kwa kuwa upanuzi au ufasili wa maana hiyo hutokana na mazingira halisi ya mawasiliano kama inavyoonekana katika Data Na. 3.

3. *Unaweza kunipitishia chumvi?*

Chanzo: Yule (1996: 101).

Kulingana na Data Na. 3, kisemantiki sentensi hiyo ina maana ya moja kwa moja kuhusu swali linalouliza uwezo wa mtu kupitisha chumvi. Hata hivyo, katika muktadha wa kipragmatiki, sentensi hiyo inaweza kufasiliwa kama ombi la kupitishiwa chumvi. Hapa inaonekana wazi kuwa maana ya kipragmatiki hujengwa juu ya maana ya kisemantiki na kisha kupanuliwa na muktadha wa mawasiliano. Aidha, maana za kisemantiki huchanuza maana za kipragmatiki kutokana na mwingiliano wa maarifa ya kisemantiki na ujuzi wetu wa ulimwengu ikiwa ni pamoja na muktadha wa mazungumzo kama inavyodhihirika katika Data Na. 4.

4. *Si mara yako ya kwanza kuchelewa.*
   Chanzo: Hansen na Visconti (2009: 54).

Kutokana na Data Na.4, sentensi hiyo kisemantiki inamaanisha mtu hufika baada ya muda uliopangwa kupita. Hata hivyo, kipragmatiki sentensi hii inaweza kutafsirika kama kitendo cha kulaumu, kukosoa au kuonya mtu aliyechelewa. Tafsiri hii inategemea uelewa wa maana ya msingi ya maneno yaliyotumika ambayo baadaye hufasiliwa upya kulingana na muktadha wa mawasiliano. Hivyo, semantiki na pragmatiki ni nyanja zinazokamilishana kwa kuwa pragmatiki inahusika na jinsi tunavyotumia lugha katika mawasiliano. Pia, semantiki hutoa ingizo la msingi kwa tafsiri za kipragmatiki na pragmatiki huhusisha maana iliyokusudiwa na mzungumzaji katika muktadha lakini maana hiyo haiwezi kupatikana bila kuwapo kwa msingi wa maana ya kiisimu (Griffiths, 2006; Yule, 2006; Hansen, 2008). Vilevile, Bublitiz na Norick (2011) wanashadidia kuwa semantiki na pragmatiki ni taaluma zinazokamilishana kwa kuwa semantiki hutoa ingizo kwa pragmatiki. Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa semantiki na pragmatiki ni matawi ya isimu yanayohusiana na ni vigumu kuyawekea mipaka kiutendaji. Maana ya kipragmatiki hutokana na mwingiliano kati ya maana ya kiisimu na muktadha wa matumizi. Hivyo, tafsiri ya kipragmatiki haiwezi kujitegemea bila msingi wa kisemantiki. Mtu hawezi kujua maana ya kimuktadha bila kujua maana ya kiisimu. Hii ina maana kuwa ili mtu aweze kufasili maana ya kipragmatiki lazima kwanza awe na uelewa wa maana ya kisemantiki. Kwa mantiki hiyo ni kwamba pragmatiki haijitegemei yenyewe bali hujengwa juu ya msingi wa semantiki ambapo uelewa wa maana ya kimuktadha unategemea kwanza uelewa wa maana ya kiisimu, jambo linaloonesha uhusiano wa utegemeano kati ya matawi haya mawili ya isimu. Hivyo, semantiki na pragmatiki ni matawi ya isimu ambayo yana uhusiano wa karibu.

Kutokana na data pamoja na ufafanuzi wa wataalamu hao, ni dhahiri kuwa maana ya kipragmatiki huibuka kutokana na mwingiliano kati ya maana ya kisemantiki na muktadha wa matumizi. Muktadha husaidia kukamilisha maana ya kipragmatiki kutokana na sifa bainifu za kiambo cha kiisimu. Hivyo, pragmatiki hutegemea semantiki kwa kiwango kikubwa katika ujenzi wa maana za kimuktadha. Kwa hiyo, semantiki na pragmatiki ni matawi ya isimu yanayohusiana kwa karibu ambapo semantiki hutoa msingi wa maana ilhali pragmatiki huupanua na kuuboresha katika muktadha wa matumizi ya lugha. Kwa mantiki hiyo, semantiki huchangia katika ujenzi wa maana za kipragmatiki, jambo linaloifanya lugha kueleweka kwa ufanisi zaidi.

3.4 Semantiki na Pragmatiki Huchunguza Maana za Ishara kwa Kutumia Simiotiki

Semantiki na pragmatiki huchunguza maana ya umbo au ishara kwa kutumia dhana ya simiotiki. Uchunguzi huu wa maana ya ishara kupitia simiotiki ndiyo unaobainisha uhusiano uliopo kati ya semantiki na pragmatiki. Kwa mujibu wa Ferdinand de Saussure (1974), simiotiki ni taaluma inayojihusisha na uchunguzi wa mifumo ya ishara katika mawasiliano ya kijamii. Vilevile, Hassan (2011) anaeleza kuwa simiotiki ni sayansi inayochunguza mifumo au miundo ya ishara pamoja na

michakato yake katika mawasiliano. Kimsingi, pragmatiki ni sehemu ya simiotiki kwa kuwa huchunguza uhusiano kati ya ishara na watumiaji wake katika muktadha halisi wa mawasiliano. Hivyo, pragmatiki hujikita katika namna mzungumzaji na msikilizaji wanavyotafsiri maana ya lugha kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa upande mwingine, semantiki hutumia simiotiki kuchunguza maana ya moja kwa moja ya ishara za lugha. Maana hii huhusisha uhusiano uliopo kati ya ishara (neno au sauti) na kitu kinachorejelewa.

Katika mtazamo wa kisemiotiki, maana ya ishara haiishii kwenye maana ya moja kwa moja pekee bali hutegemea pia matumizi yake katika muktadha maalumu wa kijamii. Hivyo basi, semantiki na pragmatiki hukamilishana katika kufafanua maana ya ishara za lugha kama inavyoonekana katika Data Na. 5.

5. *Moshi*

Chanzo : Eco (1976 : 17)

Kisemantiki Data Na. 5, ishara ‘moshi’ humaanisha kuna moto. Kiasili, moshi hutokana na moto. Hata hivyo, kipragmatiki ishara ‘moshi’ inaweza kutumika kutengeneza maana mpya za ziada kulingana na muktadha wa mazungumzo. Kwa mfano, katika muktadha wa ‘uchaguzi wa papa’ambaye ni kiongozi wa dini ya Kikristo (Kikatoliki), ishara ya‘moshi mweupe’ huibua maana ya kupatikana kwa papa mpya ambapo ‘moshi mweusi’ huonesha kuwa bado papa hajapatikana. Aidha, katika muktadha wa msituni, neno ‘moshi’ linaweza kumaanisha hatari kutokana na kuungua kwa msitu. Maana hiyo ya kimuktadha haipatikani moja kwa moja bali hufasilika kwa kuzingatia wa matumizi yake katika muktadha husika. Hivyo, pragmatiki kupitia semiotiki husaidia kuelewa maana fiche inayokusudiwa na mzungumzaji kupitia ishara za lugha. Kutokana na uhusiano uliopo kati ya ishara na maana inayowakilishwa, ni dhahiri kuwa semantiki na pragmatiki zina uhusiano wa karibu unaokamilishana kwa kuwa taaluma zote hutumia ishara (simiotiki) kufasili maana zake. Kwa mujibu wa Saeed (2006), semantiki na pragmatiki ni nyanja zinazohusiana kwa kuwa zote hujihusisha na uchunguzi wa maana za alama au ishara zinazowakilisha vitu, dhana na matukio mbalimbali yaliyopo ulimwenguni. Kwa msingi huo, ishara za kiisimu zinaweza kufasiliwa kwa mtazamo wa kisemantiki na kipragmatiki kutegemeana na matumizi yake katika mawasiliano.

Semantiki huchunguza maana ya moja kwa moja ya ishara za lugha. Uchunguzi huu hujikita katika uhusiano kati ya ishara na kitu au dhana inayowakilishwa. Hivyo, semantiki hushughulikia maana halisi ya maneno, sentensi au ishara za lugha bila kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Kwa kuwa lugha yoyote huwa na maana, msimbo wa kiisimu hulazimika kufasiliwa kwanza katika kiwango cha kisemantiki kabla ya kupewa tafsiri ya kipragmatiki. Pia, pragmatiki hutumia simiotiki katika kuchunguza namna ishara za lugha zinavyotumika katika muktadha halisi wa mawasiliano. Kwa mujibu wa Sztencel (2018), maana ya ishara inaweza kubadilika kulingana na mazingira ya matumizi, dhamira ya mzungumzaji na uelewa wa msikilizaji. Semantiki hushughulikia uhusiano wa moja kwa moja kati

ya ishara za lugha na vitu vinavyorejelewa ilhali pragmatiki hueleza maana ya ziada inayojitokeza kutokana na matumizi ya ishara hizo katika mazingira halisi ya mawasiliano. Kwa mantiki hiyo, pragmatiki hupanua maana ya lugha kwa kuangalia matumizi yake katika mazingira mahususi ya kijamii. Hivyo, kupitia simiotiki, wanaisimu wa semantiki na pragmatiki huchunguza namna mfumo wa ishara unavyobeba maana katika mawasiliano. Kwa msingi huo, simiotiki husaidia kueleza namna maana inavyowasilishwa na kufasiliwa kupitia ishara pamoja na muktadha wake wa matumizi. Hapo ndipo semantiki na pragmatiki hukutanishwa na simiotiki katika ufasili wa maana za lugha kutokana na ishara mbalimbali zinazotumika katika mawasiliano.

4.0 Hitimisho

Kwa ujumla, semantiki na pragmatiki ni matawi muhimu ya isimu yanayoshughulikia maana katika lugha kwa mitazamo tofauti lakini inayokamilishana kiutendaji. Semantiki hujihusisha na maana za msingi za maneno, sentensi na miundo ya lugha ilhali pragmatiki huzingatia namna maana hizo zinavyotafsiriwa na kueleweka kulingana na muktadha wa matumizi. Hivyo, ili kufanikisha mawasiliano yenye uelewa mpana na sahihi, ni muhimu kuzingatia mchango wa taaluma zote mbili kwa pamoja. Uchanganuzi wa lugha hauwezi kuwa kamili iwapo utazingatia semantiki pekee bila pragmatiki au pragmatiki pekee bila semantiki kwa kuwa kila taaluma ina nafasi muhimu katika kufafanua maana inayokusudiwa katika mawasiliano ya binadamu.

Marejeleo

Birner, B.J. (2013). *Introduction to Pragmatics*. West Sussex: Wiley Blackwell.

Bublitiz, W. na Norrick (2011). *Handbooks of Pragmatics Volume 1*. Berlin: Gruyter GmbH Co. KG.

Cruse, A. (2006). *A Glossary of Semantics and Pragmatics*. Edinburgh. Edinburgh University Press.

de Saussure, F. (1974). *Course in General Linguistics*. (W. Baskin, Trans.) London: Fontana/Collins

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics.* London: Indiana University Press.

Fromkin, V., Rodman, R., Hyams, N., Amberber, M., Cox, F. na Thornton, R. (2022). *An Introduction to Language, Toleo la Kumi*. South Melbourne: Cengage Learning Australia Pty Limited.

Geeraerts, D. (2010) Theories of Lexical Semantics. New York: Oxford University Press.

Griffiths, P. (2006). *An Introduction to English Semantics and Pragmatics.* Edinburg: Edinburg University Press.

Hansen, M.M. na Visconti. J. (Wah.) (2009). *Current Trends in Diachronic Semantics and Pragmatics.* Manchester: Emerald Group Publishing Limited.

Hansen, M.M. (2008). *Particles at the Semantics/Pragmatics Interface: Synchronic and Dichronic Issues*.Oxford: Elsevier Ltd.

Hassan, B.A. (2011). *Literary Translation: Aspects of Pragmatic Meaning*. Newcastle: Cambridge Scholars Publishing

Horn, L.R. na Ward, G. (Wah.) (2006). *The Handbook of Pragmatics.* Malden: Blackwell Publishing Ltd. Inapatikana https://www.researchgate.net/publication/240908949.

Kahigi, K.K. (2019). *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili, kwa ajili ya Vyuo na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Katui, S.P. (2021). *Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Maana ya Mawasiliano katika Jukwaa la Facebook.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi.

Kreidler, C.W. (1998). *Introducing English Semantics.* London and New York: Routledge.

Kroeger P.R. (2018). *Analyzing Meaning: An Introduction to Semantics and Pragmatics.* Berlin: Language Science Press.

Kumar, A. (2019). "The Use Theory of Meaning: A Reading of Wittgenstein's Philosophical Investigations". *Journal of Emerging Technologies and Innovative Research*, Juz. 6 (5): 223-226. Inapatikana katika https://doi.org/10.5281/zenodo.4399324 www.jetir.org (ISSN-2349-5162).

Saeed, J.I (2016). *Semantics* (Fourth Edition). West Sussex: Wiley Blackwell Publishing Ltd.

Sztencel, M. (2018). *Semantics, Pragmatics and Meaning Revisited*: *The Case of Conditions*. New York: Springer.

Wittgenstein, L. (1953). *Philosophical Investigations*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Yule, G. (1996) *Oxford Introductions to Language Study*: *Pragmatics.* New York: Oxford University Press.

Yule, G. (2006). *The Study of Langauge* (Toleo la Nne). London: Cambridge University Press.